

Pambazuko

Toleo Namba 064

Jumatatu Machi 4-10 2024

Kila Mtanzania adaiwa 1.4m/-

•Nchi yadaiwa Sh. triloni 87.47

Naita tena na tena;
Kikwete, Kikwete

UK. 5



Jicho la Tai



KURASA 9 NDANI ZAMLILIA RAIS ALHAJ MWINYI



JISAJILI HAPA: Andika neno **HABARI** na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Sisi hatumlilii Rais Mwinyi, tunasherehekea

MAIISHA ya Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Awamu ya Pili wa Tanzania kwa miaka 10; kuanzia 1985 hadi 1995, yamekoma hapa duniani Februari 29, mwaka huu, 2024.

Rais Samia Suluhu Hassan aliitangazia dunia kwamba kifo cha Alhaj Ali Hassan Mwinyi kilisababishwa na ugonjwa na kwamba alikuwa akipatiwa matibabu nje ya nchi na baadaye kurejeshwa Tanzania, lakini uhai wake ukakoma wakati akiendelea na matibabu katika Hospitali ya Mzena, Dar es Salaam.

Pambazuko tunatoa pole nyingi kwa Watanzania, familia, ndugu jamaa na marafiki wote wa kiongozi huyo wa marafiki wote wa kiongozi huyo wa nchi ambaye utu wake haujawahi na huenda usifikiwe na kiongozi yeyote aliyekuwepo na hata watakaokuja.

Katika uongozi wa miaka 10 ya urais wa Tanzania, Rais Mwinyi amethibitisha kuwa siyo lazima kuwa mbabe, kukosa utu, kuonea watu na hata kuamuru kuua binadamu wenzako kwa kuwa tu una mamlaka makubwa ya kufanya hivyo.

Kwamba katika uongozi, lazima wapo watu unaowaongoza watakupinga, hawatakuielewa na pengine, kwa kiburi na hulka zao, watakukebehi, kukufanyia dhihaka, kukukejeli na hata kukutusi, na kwa mamlaka makubwa unaweza kuamuru wapate “adhabu” za wazi na hata kificho.

Historia ya uongozi wa Tanzania imeshuhudia hayo, lakini kwa Rais Mwinyi, hakuna taarifa zenye kuthibitisha kuwa aliweka utu pembeni na kuwaadhibu “waliomkera” zaidi sana tumeshuhudia akisamehe wote waliokuwa wakimsumbua.

Huyu ni kiongozi aliyesamehe hata kijana aliyethubutu kumzaba kibao Rais Mwinyi wakati akihutubia, lakini alimsamehe na kumuombea msamaha kwa wengine wote waliokasirishwa na ujinga ule.

Huyu ndiye Mwinyi anayetambulika kwa kugoma kulipa kisasi wala kurejesha chuki kwa waliompaka matope.

Hata alipoguswa kwa kueleza kuwa uongozi wake ulikuwa dhaifu, kwa vigezo yya waliodai hivyo, hakuthubutu kufungua mdomo wake kukemea wala kujitetea. Aliacha hilo lipite, huku yeye akichapa kazi kuwatumikia Watanzania.

Katika kitabu chake, kilichopewa jina la Mzee Rukhsa, ameeleza masaibu mengi aliyokumbana nayo wakati akifanya kazi za umma na hata kufukuzwa ndani ya nyumba ya serikali na mmoja wa mawaziri wenzake na kupokwa hata baadhi ya mali zake halali, lakini hakuwahi kulipiza.

Mwenye matendo haya ni nani? Iweje sasa sisi tuanze kumlilia mtu wa namna hiyo, tena akiwa na miaka mingi zaidi kuliko inayotajwa na Vitabu Vitakatifu; Biblia na Quran, kuwa ndiyo mwisho wa mwanadamu kuishi?

Sisi Pambazuko tumekataa kumlilia Rais Mwinyi na badala yake tunaomboleza maisha yake kwa furaha kuu kwamba ametimiza wajibu wake wa uongozi na maisha ya dunia hii iliyojaa dhuluma, uonevu, wivu, visasi; vitu ambavyo yeye aligoma kuviishi.

Lala Salama Rais Ali Hassan Mwinyi.

MVUA HAIWEZI KUTUZUIA ...



BAADHI ya viongozi wa juu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), wakiongozwa na Freeman Mbowe, mwenyekiti wa chama hicho (aliyevaa kofia nyekundu mbele), wakiandamana Jumanne iliyopita katika mitaa ya Jiji la Arusha. Maandamano hayo ya amani ya chama hicho yanaendelea mikoa yote ya Tanzania yakibeba kibwagizo kikuu; “maisha magumu kwa wananchi yatatuliwe.” (Picha kutoka mtandao wa X).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno “**HABARI**” kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno “**HABARI**” na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



Nimeambiwa kwamba wapo wanaoona uongozi wa serikali umekuwa lelegele, lakini naomba kuwahakikishia kuwa tuko imara na tunafanya kazi kwa nguvu na uwezo wetu wote kwa imani ya kuwakwamua Watanzania – Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Awamu ya Pili wa Tanzania (1985-95).

Tangazo

Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

Mhariri Mkuu,
Oktoba, 2023

Changia Pambazuko liendelee

WAJUMBE wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufuraha kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakituma fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokuwa zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukua Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeviza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yameweka wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majaraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kumarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kusuzwa, lakini hasi kubaliana na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchagia, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sawa ya "asante" kutoka kwetu.

Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263

Ukituma mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandika: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.

Lipa kwa Simu

Lipa kwa kuscanner



Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI



Naita tena na tena; Kikwete, Kikwete

Na Igo AI

OKTOBA 16, mwaka wa jana – 2023, kupitia gazeti hili la Pambazuko, toleo nambari 50, Mzee Tai alimuasa Rais (mstaafu) Jakaya Halfani Mrisho Kikwete jambo zito, muhimu na lenye utu.

Mzee Tai aliamua kufanya hivyo kwa mambo makubwa mawili; moja akiamini kwamba anapaswa kutenda hivyo kwa kuwa Jakaya ni rafiki yake, mzee wake, kiongozi wake, na zaidi sana ni mtani wake. Tai anatoka Mwanza, ni Mkusuma na Jakaya ni Mkwere, anatoka Pwani.

Utani wa Wasukuma na Wakwere, ni ule wa kujenga, kuchekeshana na kusaaidiana katika masuala anuai; iwe sherehe na hata kwenye majanga.

Sababu ya pili kwa Tai kuamua kubeba jukumu la kumuasa Jakaya, ni Msingi wa Neno la Mungu. Kwamba bin-Adamu wanapaswa kuasa wenzao. Kwamba endapo mtu anaona mwenzake amekengeuka, basi anapaswa kutimiza matakwa ya Allah, ili kurekebisha.

Basi, Tai alimuasa Jakaya Halfani Mrisho Kikwete kuwahi Afrika Kusini, kwenda moja kwa moja hadi Hospitali ya Milpark, iliyopo Jiji la Johannesburg, Afrika Kusini, Barabara inayoitwa - 9 Guild Parktown, kumjulia hali Edward Ngoyai Lowassa, ambaye alikuwa amelazwa hospitalini hapo kwa matibabu mahsusi.

Tai, pamoja na kutimiza wajibu wake wa kuasa, pia alisukumwa na nafsi yake kufanya hivyo, kwa kuwa alitamani kuona urafiki uliokuwepo kati ya Jakaya na Lowassa uliovuka viwango vya udugu – unarejea na kumea. Walishibana kwelikweli wawili hawa.

Tai anadai kuwa na taarifa za wawili hao kufikia hatua ya kupeana yamini na kuweka ahadi zinazodaiwa kuwa maapizo.

Hata hivyo, baada ya Jakaya kukaidi



Rais mstaafu, Jakaya Kikwete

ushauri na maono haya, Mzee Tai aliamua kumuacha na kumuombea kwa Mungu ili siku ije ya rafiki huyo wa Lowassa, aende kumsabahi na kumjulia hali swahiba wake.

Lakini kumbe Tai, kama ilivyo wengine, hawajui kesho yao, wala hawatambui mipango ya Allah, Lowassa akarejeshwa Dar es Salaam na baada ya muda, aliyemuumba - akamchukua.

Tai anasema Jakaya kwa Kisukuma ni “za nyumbani,” hivyo anaona fahari pia kumwambia nini kinajiri nyumbani, hasa baada ya kifo cha Lowassa.

Baada ya kifo cha Lowassa, mengi yanazungumzwa kuhusu ukaribu wao uliokatizwa na dalili za wazi za mpasuko na hata kudhihirika siku za kuaga mwili wa Lowassa, kwamba Jakaya alikuwa na nafasi kubwa ya kutambulishwa na akabaki amejinamia kama kijana wa Tai aliyenyesha mvua.

Hata hivyo, Tai anabaki na kubwa moja baada ya kutokea hayo; Jakaya Halfani Mrisho Kikwete ana siri kubwa moyoni, kichwani juu ya ajali ya kisiasa ya Lowassa.

Unaweza kuwasiliana na Mzee Tai kupitia namba ya mwandishi wake; 0754 020880

Habari

Kila Mtanzania sasa adaiwa 1.4m/

Na Tryuckia MFINANGA

MIRADI mikubwa ya kimkakati nchini Tanzania, imepaisha deni la taifa hilo hadi kufikia Shilingi trilioni 87.47.

Kiasi hicho cha fedha za deni, endapo kitagawanywa kwa mwananchi mmoja mmoja; basi kila Mtanzania, bila kujali umri, atakuwa anadaiwa Shilingi milioni 1.4, Pambazuko linaeleza.

Hesabu hiyo inatokana na Shilingi trilioni 87.47 kuganywa kwa idadi ya Watanzania, ambao inaeleza na serikali kufikia milioni 62. Idadi hii ni ile inayotajwa na Takwimu za Tanzania kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

Deni hilo la Taifa la Tanzania ni ongezeko la zaidi ya Shilingi trilioni 12 au asilimia 17, hadi kufikia Shilingi trilioni 87.47 kufikia Desemba 2023.

Pambazuko limebaini kuwa deni la Serikali ya Tanzania lilipanda kwa kasi kubwa katika kipindi cha miezi sita; Desemba 2022 hadi Juni 2023 - kutoka Shilingi trilioni 74.75 hadi kufikia trilioni 80.33.

Gasiti hili pia limetambua kuwa deni hilo limeongezeka kwa Shilingi trilioni 12 kwa kipindi cha mwaka mmoja, kutoka Januari, 2023 hadi Februari 2024.

Imethibitika kuwa kukua kwa deni hilo pia kunasukumwa na matumizi makubwa na mengine ya "hovyoy", yanayofanywa na baadhi ya watendaji wa serikali, ikiwamo kupandisha bei ya huduma na hata ununuzi wa bidhaa kutoka nje ya nchi, kwa kutumia dola ya Marekani.

Pambazuko linatambua kuwa miongoni mwa hasira za wazi alizowahi kuonesha Rais Samia Suluhu Hassan, ni kuongezwa kwa bei ya malipo ya ndege kiasi cha kutamka neno "stupid (ujinga) kwa sauti ya hasira baada ya kuamini kuna "upigaji" uliofanyika katika ongezeko hilo.

Katika kukamilisha malipo ya ununuzi



Rais Samia Suluhu Hassan

wa ndege ya mizigo (cargo), Tanzania ililazimika kuongeza zaidi ya Shilingi bilioni 110. (dola za Marekani milioni 49), ambazo hazikuwamo kwenye ankara wala mkataba wa awali.

Ofisi iliyowasilisha ankara Ikuu baada ya kupita miaka miwili na nusu ya mkataba wa awali, ilimuonesha Rais Samia kwamba ongezeko hilo lilitokana na kupanda kwa vifaa vya kutengeneza ndege hiyo, pamoja na kuwepo kwa mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19.

Mbali na hasira za Rais Samia katika ununuzi wa ndege hiyo, pia amethibitisha kuwepo upigaji mwingine mkubwa wa fedha kupitia ununuzi wa vishikwambi (laptop) vya kuchukua taarifa wakati wa zoezi la sensa ya watu na makazi. Sensa ilifanyika mwaka 2022. Ankara ya vishikwambi hivyo iliongezeka kwa Shilingi bilioni 10. Nazo serikali ililipa.

Hata hivyo, katika mazingira hayo, Rais Samia hakuchukua hatua kali zinazofahamika kwa umma, kulingana na kauli zake.

Mkt. Lenny Kasoga, mchumi mboenzi na mhadhiri wa vyuo vikuu ndani na nje ya Tanzania, anasema ongezeko hilo kubwa la deni, linagubikwa na mambo

Falsafa za Askofu Bagonza a kimlilia Alhaji Mwinyi

RAIS Mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi ameondoka. Umri wa karne moja umetimia ukihesabu na muda wa mimba yake. Ndo maana tunazuia utoaji mimba kwa sababu anakuwa ni mtu yule! Kwa heri Mzee Rukhsa.

Nimemtafakari kwa mengi Rais Mwinyi. Huyu alionja furaha na ghadhabu ya Kamarage. Mwinyi alikabidhiwa nchi ikiwa hoi, lakini hakuwa huru kusema kuwa nchi ni hoi. Kimyakimya akaingia kazini na kiranja akiwa Butiama. Ukikooa Ikulu anasikia. Kamarage ni Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa Awamu ya Kwanza wa Tanzania.

Alipojaribu kuanza mageuzi, alikumbana vikwazo ndani na nje. Kwa ndani kikubwa kilikuwa Kamarage. Nje Shirika la Fedha Duniani (IMF) na Benki ya Dunia. Alikemewa kama mtoto na kutungiwa kitabu na akatii. Siyo kawaida mwenye rungu kumfokea mwenye bunduki. Ilitokea na maisha yakaendelea.

Tukiwa wanafunzi vyuo vikuu, tukapimana vifua na Mzee Mwinyi. Tukagoma na kuandamana. "Punch" akampunch rais na kusababisha kifo cha punch. Vyuo vikafungwa, tukauza blanketi kupata nauli ya kwenda nyumbani. Wengine hawakurudi mpaka leo. Tunamtamani Punch lakini hatorudi. Mzee Mwinyi msalimie Punch huko uendako.

Mwinyi alizima ndoto za wengi. Kabla yake hakuna aliyedhani wala kuota kama kuna Tanzania bila Kamarage. Ikawezekana. Kwa uungwana wake akagawa madaraka: Sehemu akawa nayo Kamarage; nyingine akampa Mrema; na nyingine Mama Sitti. Tukavuka.

Ameishi na maraisi wote waliowahi kutuongoza. Hata walipotofautiana, aliwaheshimu na kuwasifia wote. Akamlinganisha Kamarage na Mlima Kilimanjaro na yeye ati, ni kama kichuguu. Akampokea bila kinyongo Ben



Mkapa hata kama hakumtegemea awe mrithi wake.

Alimpenda JK (Jakaya Kikwete) kuliko hata JK alivyojipenda. Akamsifia JPM (John Pombe Magufuli) kuwa amefanya makubwa kuliko wote waliomtangulia wakijumlishwa pamoja! Akachombeza "kwa nia njema" kuwa katiba itazamwe ili JPM aendelee. Alimpenda sana SSH (Samia Suluhu Hassan) mpaka akachombeza "mwanamke aliyekuzidi kwa shughuli hata kwa kimo, ni mama yako huyo."

Rais Mwinyi aliutikisa na kuuimarisha Muungano kwa namna yake. Alizaliwa Tanganyika. Akakulia Zanzibar. Akatumikia wizara za hayati Tanganyika. Akawa Rais wa Zanzibar. Akawa Rais wa Muungano. Akaishi Bara kama mstaafu. Akafia Bara. Akazikwa Zanzibar. Angekuwa Mkristo tungenema atafufukia alipofia - Bara!

Pumzika kwa amani Alhaj Ali Hassan Mwinyi.

Ulianza kutuongoza wakati wa uhaba wa kila kitu. Umeondoka wakati wa uhaba wa sukari, umeme na furaha.

Mwandishi wa Tanzia hii ni Dkt. Benson Bagonza, Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Jimbo la Karagwe.

Tutaonana Tena



Baadhi ya matukio ya katika shughuli ya kuaga mwili wa Ali Hassan Mwinyi, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili ya Tanzania aliyefariki dunia Februari 29, 2024. Kiongozi huyo alizikwa siku nne - Machi 3, baadaye kijijini kwake Mangapwani, Unguja, Zanzibar - (Picha kutoka Ikuilu).



Kila Mtanzania sasa adaiwa 1.4m/

Inatoka Uk. 6

mengi, ikiwamo ufisadi na ubadhirifu mwingine.

Mchumi huyo anabainisha kuwa fedha nyingi za ufisadi hupitia kwenye michakato ya miradi mikubwa, hasa inayotekelezwa kutoka kwa kandarasi nje ya nchi.

Kamati ya Bunge ya Bajeti, katika ripoti yake ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kuanzia Februari 2023 hadi Januari 2024, imesema kuwa deni la taifa linajumuisha takriban asilimia 35 ya Pato la Taifa la Tanzania kwa mwaka.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Daniel Sillo amesema kuwa ongezeko la deni la serikali limechangwa na ongezeko la malipo ya fedha za miradi ya kimkakati kama vile barabara, reli, viwanja vya ndege, maji na usambazaji wa umeme.

Hata hivyo, wachumi pia wameliambia

Pambazuko kwamba deni la nje limeongezeka kutokana na mabadiliko ya viwango vya ubadilishaji fedha pamoja na riba ya mikopo.

Deni la nje hadi wiki iliyopita lilikuwa Shilingi trilioni 56.79 wakati deni la ndani ni Shilingi trilioni 30.67.

Imebainika kuwa asilimia 28 ya deni la nje lina riba inayobadilika kulingana na soko, huku asilimia 71.7 ikiwa na riba isiyobadilika.

Katika bajeti ya serikali inayoendelea kutumiwa – ya mwaka huu wa fedha 2023/24, zaidi ya Shilingi trilioni 10.48 zilitengwa ili kuhudumia deni hilo linaloongezeka kila uchao – ikiwa litachelewa kulipwa. Bajeti ya Tanzania kwa kipindi hiki ni Shilingi trilioni 44.38.

Kiasi hicho ni ongezeko la asilimia 16.4 kutoka Shilingi trilioni 9 zilizotengwa kuhudumia deni katika bajeti ya mwaka uliopita, 2022/2023.



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Hadithi ya Mzee Mwinyi ituachie funzo

Na Rashid MMTAGARUKA

NIKIULIZWA popote pale kuwa ni ujumbe gani muhimu aliouacha Rais (mstaafu) Alhaj Ali Hassan Mwinyi, bila kupepesa macho nitanukuu kauli ifuatayo.

“Maisha ya mwanadamu ni hadithi tu hapa ulimwenguni, basi ewe ndugu yangu kuwa hadithi nzuri kwa hao watakaosimuliwa hilo ndo ninaloliomba”

Kifo cha Mzee Mwinyi kilichotokea Alhamisi - Februari 29, 2024 na kutangazwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kinatimiza idadi ya wanasiasa wanne kati ya watano waliopata kuiongoza nchi yetu katika nafasi ya urais kuaga dunia.

Wa kwanza kufariki alikuwa ni Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa Kwanza wa Tanzania aliyetutoka Oktoba 14, 1999 nchini Uingereza alikokwenda kutibiwa akiwa na umri wa miaka 75.

Baada ya Mwalimu Nyerere, Julai 24, 2020, Watanzania wakapokea taarifa ya ghafla ya kifo cha Rais (mstaafu)- wa awamu ya tatu, Benjamin William Mkapa, aliyefariki dunia jijini Dar es Salaam akiwa na umri wa miaka 81.

Mwaka mmoja baadaye, Machi 17, 2021 taifa likagubikwa tena na msiba wa Rais Dkt John Pombe Magufuli kilichotokea hospitali ya kumbukumbu ya Emilio Mzena jijini Dar es Salaam alikokuwa akipatiwa matibabu. Huyu alikuwa bado madarakani.

Akitangaza kifo cha Mwinyi, Rais Samia alisema kimetokea katika Hospitali ya Mzena, alikokuwa akipatiwa matibabu ya ugonjwa wa saratani ya mapafu.

Yako mambo mengi ya kusimulia katika maisha ya Mzee Mwinyi - almaarufu Mzee Rukhsa, aliyefariki akiwa na umri wa miaka 98, ambayo viongozi wa vyama vya siasa na serikali wanaweza kujifunza.

Kwa mfano tuna cha kujifunza kwenye



Rais Mwinyi

kisa cha waziri mmoja wa Serikali ya Mwalimu Nyerere kumwambia Mwinyi ahame haraka kwenye nyumba ya serikali aliyokuwa anaishi huko Oysterbay, Dar es Salaam, baada ya kutangaza kujiuzulu kwa hiyari yake nafasi ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mwaka 1977 kufuatia sakata la mauaji mkoani Shinyanga.

Baada ya kupata msaada wa kuhamia kwenye nyumba mojawapo ya rafiki yake, Alhaj Kitwana Kondo huko Temeke, waziri huyo alijikuta anajimilikisha baadhi ya vifaa vya ujenzi vya Mwinyi zikiwemo bati.

Mungu siyo Athumani, miaka michache baadaye Mzee Rukhsa akawa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Yule waziri akaingwa na hofu akikumbuka jinsi alivyomfanyia Mwinyi alipojiuzulu uwaziri. Akatafuta bati mpya kwa idadi zisizosemeka na kwenda kumrejeshea huku akitanguliza kumuomba radhi.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa, Mzee Rukhsa alipokea mzigo huo na kuhesabu kiasi cha bati alichokuwa amekiacha pale Oysyerbay miaka hiyo, na kumweleza hizo nyingine arudi nazo, siyo haki yake, hataki dhulma.

Ndiyo maana nasema hadithi ya mzee Mwinyi ituachie funzo.

Kenya**‘Baba’ aunganisha nchi akigombea AU**

Na Mwandishi WETU

RAILA Amolo Odinga, sasa amekuwa “lulu ya ajabu” kwa kuunganisha Wakenya bila kujali mrengo wa siasa, kabila na maeneo.

Kiongozi huyo wa muungano wa vyama mbalimbali nchini humo, Azimio la Umoja, amewakutanisha Rais William Ruto na mtangulizi wake, Uhuru Kenyatta na kuzungumza kuhusu “kupigania Kenya.”

Kipindi hiki hawaungani kusaka uongozi wa kisiasa ama kuungwa mkono na Wakenya pekee, bali ni kuhakikisha Raila anashinda nafasi ya Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika (AU).

Tayari kampeni zimeanza na Rais Ruto na Uhuru wametembelea nchi jirani zinazopiga kura kumpata mwenyekiti huyo wa AU.

Wiki iliyopita, Rais Ruto akiwa ameongozana na mgombea wa AU, Raila, walimfikia Rais wa Uganda, Yoweri Museveni kumshawishi ili nchi yake impigie kura Raila wakati utakapofika.

Mbali na Rais Ruto kwenda Uganda, Uhuru alisafiri kutoka Nairobi, Kenya hadi Zanzibar, Tanzania na kukutana na Rais Samia Suluhu Hassan kwa lengo hilo hilo la kuomba Tanzania impigie kura Raila.

Pamoja na kwamba mazungumzo hayo yalielezwa na Ikulu kuwa ni “binafsi,”

Pambazuko limepata taarifa kuwa yalikuwa yakihusu maombi ya Rais Ruto na Raila, kuungwa mkono na Tanzania ili Raila apate kuibuka mshindi kwenye kinyang’anyiro cha mwenyekiti wa AU.

Rais Ruto akiwa na Raila wao walimfuata Museveni shambani kwake, Kisozi ambako walifanya m a z u n g u m z o

hayohayo, inagwa Ikulu ya Uganda nayo ilidai viongozi hao walizungumza zaidi kuhusu ushirikiano wa maendeleo baina ya nchi hizo mbili za Afrika Mashariki.

Raila ambaye pia ni waziri mkuu wa zamani wa Kenya, aliwahi kuwa Mkuu wa Maendeleo ya Miundombinu wa AU mwaka 2018. Majukumu hayo yalikoma mwaka jana, Februari 2023.

Nafasi ya mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika ni nafasi ya mtendaji mkuu wa Tume ya Umoja wa Afrika, ambaye pia ni mwakilishi wa kisheria wa AU Umoja wa Mataifa.

Nafasi hiyo kwa sasa, ipo chini ya Moussa Faki Mahamat ambae ni raia wa Chad.

Ili kupata kiti hiki, marais wa nchi za Afrika hupiga kura ya siri. Mgombea anahitaji kupata angalau theluthi mbili ya kura, ambayo ni sawa na kura 36, ili kutangazwa mshindi.

Rais wa zamani wa Nigeria Olusegun Obasanjo ameunga mkono uamuzi huo wa Raila Odinga.

Hii siyo mara ya kwanza kwa Kenya kugombea nafasi hiyo ambayo ni kubwa katika Afrika. Mwaka 2017, Kenya iliwania nafasi hiyo kupitia kwa Amina Mohammed, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje.

Hata hivyo, Kenya ilishindwa na Chad iliyowakilishwa na mwenyekiti wa sasa, Moussa Faki Mahamat.



Rais Ruto -kushoto akiwa na Raila na Rais Museveni

Mwinyi kaondoka bila deni. Hatudaiani

Na Togolani MAVURA

KIONGOZI rahimu, kiongozi jasiri, kiongozi mnyenyekevu, kiongozi muungwana, kiongozi mzazi na mlezi, ndiyo sifa zinazomtambulisha Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyejaaliwa kuishi na kuona kizazi cha nne (marais wanne) cha uongozi mbele yake.

Rais Mwinyi ni kiongozi mwenye karama ya kipekee. Amekuwa Rais wa Zanzibar na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jambo ambalo ni nadra kutokea.

Utulivu wake, urahimu wake na ujasiri wake, uliwezesha Zanzibar, na baadaye Tanzania kuyaendea mageuzi makubwa ya kiuchumi na kisiasa.

Katika nyakati zote, alipokea nchi katika mazingira magumu sana. Alikuwa Rais wa Zanzibar baada ya 'kuchafuka kwa hali ya siasa Zanzibar' na kujiuzulu kwa Rais Aboud Jumbe.

Akawa Rais wa Tanzania akiipokea nchi ikiwa 'hoi bin taaban' kiuchumi, ikiwa haina bidhaa madukani, wala akiba ya fedha za kigeni.

Katika nyakati zote mbili, alipokea dhima kwa unyenyekevu mkubwa, hakulaumu waliomtangulia, alilinda stara yao, na alifanya mageuzi makubwa bila kubeza yaliyokwisha fanyika.

Rais Mwinyi ameonesha kuwa ujasiri na uamuzi mgumu unaoweza kupatikana bila ya lugha kali, mkono wa chuma na kumwaga damu za watu.

Alifungua uchumi wa Zanzibar, na akafungua uchumi na siasa za Tanzania. Ndiye aliyeruhusu uchumi wa soko kupitia 'Azimio la Zanzibar' na ndiye aliyenda Tume ya Nyalali, kuruhusu Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa na kuruhusu Uhuru wa Habari na vyombo binafsi vya habari.

Ni wakati huo, rais akaanza kuandikwa, kujadiliwa hadharani na hata



Rais Mwinyi

kuzushiwa, wakati huo tukianza na gazeti la Motomoto.

Rais Mwinyi anabaki kuwa kielelezo cha uwajibikaji nchini Tanzania. Alionesha uwajibikaji kwa mfano alipojiuzulu bila shuruti wala manung'uniko baada ya kadhia ya mauaji kule Shinyanga.

Wakati wa urais wake, aliwahi kuvunja Baraza la Mawaziri kuonesha kuwajibika kwa umma kutokana na tuma mbalimbali zilizoikabili serikali yake.

Rais Mwinyi alikuwa mwanademokrasia. Itakumbukwa uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi baada ya kurejeshwa mfumo wa vyama vingi ulifanyika jijini Dar es Salaam, ukiwa ni uchaguzi mdogo wa udiwani na mgombea wa upinzani Dkt. Masumbuko Lamwai wa NCCR alishinda na alitangazwa. Tukawa na diwani wa kwanza kutoka upinzani.

Hakika, maisha yake ni funzo kubwa kwetu sote. Ametuachia alama na sadaka zinazoishi. Ametuachia hadithi nzuri.

Alikuwa mtu nadra. Amefariki siku nadra ya tarehe 29 Februari ambayo huja mara moja katika miaka minne.

Hatudai. Hatumdoi.

Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Hayati Mheshimiwa Rais Ali Hassan Mwinyi mahala pema peponi.

Mwandishi wa makala haya na tanzia, Togolani Edriss Mavura ni Baloxi wa Tanzania, Korea Kusini.

Tanzia

Mwinyi kaacha hazina, tuikumbatie

Na Jesse KWAYU

MUNGU akimjalia binadamu yeyote Mumri wa miaka 98 ni baraka kubwa.

Ni wachache sana wanaopata baraka ya kupata umri huo. Ukifika makaburini kokote na kusoma maandishi kwenye utambulisho wa kila kaburi, utagundua kwamba watu wengi hawaishi umri huo mrefu.

Kujaliwa umri mrefu ni baraka, lakini pia ni neema kama anayepata anakuwa na uzee mwema. Rais Mstaafu Ali Hassan Mwinyi ambaye alitangulia mbele ya haki jioni ya Februari 29, mwaka huu, ni miongoni mwa watu wachache ambao Mungu amewakarimu neema ya uzee mwema ulioshiba miaka.


Rais Mwinyi alikuwa mtu rahimu, walau kwa macho ya kibinadamu. Wakati taifa likiomboteza msiba huu wa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, umma umepata wasaa wa kumfahamu kiongozi huo alikuwa mtu wa namna gani.

Kiongozi huyu aliyeingia madarakani zama za mfumo wa chama kimoja cha siasa mwaka 1985 na kuhitimisha muhula wake wa kwanza yake mwaka 1995, amecha nyuma hazina kubwa ya elimu kuhusu uongozi, utu, uvumilivu na kikubwa ya vyote moyo na roho ya kusamehe.

Kuna usemi maarufu kwamba huwezi kumfahamu vizuri mtu hadi pale unampomjaribu kwa mambo mawili, madaraka na mali au pesa.

Mzee Mwinyi ambaye alijipatia jina la Mzee Rukhsa kutokana na kuridhia mambo mengi, ni miongoni mwa viongozi wakuu katika Bara la Afrika wanaoweza kutajwa kwamba alifaulu mtihani huo.

Kwamba madaraka na mal au pesa havikumjaza kiburi kiasi cha kupoteza hulka yake ya uungwana, uvumilivu na



roho ya kusamehe.

Nitafanya rejea ndogo hapa ambayo binafsi nilishuhudia. Mwaka 1990 tulikuwa wanafunzi wa shahada ya kwanza katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Wakati huo Rais Mwinyi alikuwa anahitimisha ngwe ya kwanza ya miaka mitano ya utawala wake. Alikuwa ndiye Mkuu wa Chuo. Zama zile, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiye alikuwa Mkuu wa Chuo hicho, tangu zama za Mwalimu Julius Nyerere.

Kukawa na mgomo wa wanafunzi ambao ulikwenda kwa muda mrefu. Mgomo huu ulikuwa umejikita katika madai ya wanafunzi juu ya kudorora kwa huduma katika chuo hicho.

Majengo yalikuwa yamechakaa, huduma za kitaaluma zilikuwa zimeathirika pakubwa hii ikichangiwa na mageuzi ya mfumo wa uchumi ambayo yalikuwa yamekwisha kuanza nchini juu ya kuchangia gharama za huduma za kijamii kama elimu.

Katika mgomo huo, makamu mkuu wa chuo wakati huo, Profesa Geoffrey Mmari alialikwa na Baraza la Wanafunzi waliokuwa wamekutana kwa zaidi ya wiki mbili mfululizo, wakijadili hali ya kuzorota kwa hali ya huduma katika chuo hicho.

Katika Baraza hilo, Profesa Mmari alitumwa na Baraza kwenda kumleta

Inaendelea Uk. 13

Mwinyi kaacha hazina, tuikumbatie

katoka Uk. 12

Mtu ambaye angejibu maswali ya wanafunzi kuhusu kuzorota kwa hali ya huduma. Profesa Mmari alikwenda kumwita Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu wakati huo, Joseph Ngonyani.

Ngonyani alifika na timu ya wakurugenzi kutoka wizarani, aliwekwa kiti moto akitakiwa aeleze jinsi wanavyopitisha bajeti ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Baada ya vuta nikuvute iliyodumu kwa muda pale chuoni, Katibu Mkuu huyo akijaribu kujieleza, majibu yake hayakukata kiu ya wanafunzi.

Uongozi wa wanafunzi, chini ya Daruso ulimtamkia Ngonyani kuwa ameshindwa kujibu maswali yao, hivyo wakamuagiza aende kumleta Mkuu wa Chuo hii aje kujibu maswali yao. Kikao kiliahirishwa na wanafunzi wakaanza kutoka nje na kumuacha Katibu Mkuu na timu yake pale.

Hata hivyo, baadaye taarifa ililetwa chuoni kwamba Mkuu wa Chuo, yaani Rais Mwinyi alikuwa tayari kuja kuzungumza na wanafunzi endapo tu “fujo zingetulia.”

Hakika hakukuweko na fujo. Profesa Mmari alitumwa tena kwenda kwa Mkuu wa Chuo kumpa taarifa kwamba hakukuwa na fujo chuoni, yamkini alikuwa amepotoshwa na Ngonyani. Siku hiyo Ngonyani alifutwa kazi.

Hata hivyo, Mkuu wa Chuo hakufika chuoni hapo kuja kuzungumza na wanafunzi. Hali hii iliongeza muda wa wanafunzi kuwa nje ya madarasa wakidai kuwa wapo kwenye extended Students Baraza.

Hali ya mgomo huo ikazidi kubadilika, hadi ilipofika sasa ikawa ni vita ya mapambano ya fasihi kwenye mabango (literature wall) dhidi ya Mkuu wa Chuo ambaye pia ni Rais wa nchi.

Ghafla picha yenye sura ya Mwinyi ikawa deal, ikawa inatumika isivyo,



yote ikiwa ni kuwasilisha ujumbe kwake. Wenye staha na usiokuwa na staha. Kejeli na hata pengine matusi ya nguoni. Kulishuhudiwa hali wanafunzi kutokutaka kurejea madarasani.

Siku moja lilitokea tukio la kufyatuliwa kwa risasi katika eneo la chuo. Ilikeleza kwamba wanafunzi walimzingira mtu mmoja ambaye walimshuku kuwa ni mwanausalama. Katika rabsha hizo, mwanausalama huyo alijihami kwa kufyatua risasi na kufanikiwa kuponyoka. Baada ya tukio hilo hali ilizidi kuzorota siku baada ya siku.

Katika mfululizo wa hayo mabaraza ya wanafunzi, siku moja niliamka asubuhi, nilipofika eneo la Cafeteria, picha za Mzee Mwinyi nilizoziona zimebandikwa ukutani, moyo ulienda mbio, nilihisi baridi, nilipotafakari nilijua kwa hakika uwezekano wa chuo kuendelea na shughuli zake kama kawaida ulikuwa mgumu. Na kweli, siku hiyo katika taarifa ya habari ya saa saba mchana Serikali ikatangaza kukifunga Chuo Kikuu cha Dar es Salaam sehemu ya Mlimani kwa muda usiojulikana.

Wanafunzi wote waliamriwa kurejea makwao na hadi ifikapo saa 10 jioni siku hiyo wawe wamekwisha kuondoka chuoni hapo. Baadaye walitakiwa kuripoti kwa wakuu wa wilaya zao.

Tangazo



Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au

Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Mwinyi kaacha hazina, tuikumbatie

Inatoka Uk. 13

Na waliwekewa zuiu la kupewa ajira kokote ndani ya nchi.

Akizungumza na wazee wa Dar es Salaam katika utaratibu ambao zamani wakuu wa nchi walikuwa wanautumia kuhutubia taifa, Mzee Mwinyi alisema “nimetukanwa mpaka matusi ya nguoni” na wanafunzi wa Chuo Kikuu.

Hata hivyo, baada ya kupoteza mwaka mmoja wa masomo, Chuo kilifunguliwa. Wapo waliotajwa kuwa ni viongozi wa mgomo, baadhi hawakurudi kabisa, wengine walirudi baada ya muda mrefu zaidi, lakini la muhimu kulikuwa na msamaha mkubwa kwa wengi.

Kumbukumbu hii ninaoanisha na uhuru wa vyombo vya habari ambavyo serikali ya Mzee Mwinyi ilikuwa imeachia kati ya 1990 hadi 1995. Sheria zilikuwa ni zile zile za mtangulizi wake, Mwalimu Nyerere.

Lakini Mzee Mwinyi, siyo tu kuwa baadhi ya vyombo vya habari vilimvunjia heshima, kwa habari nyingi za kuzusha na kutunga, bali pia vilivuka mipaka mpaka mara nyingi kuingilia uhuru wake wa faragha.

Mzee Mwinyi alistahimili dhoruba ya mageuzi ya kisiasa, aliacha waliokuwa na kiu ya kuanzisha vyama vya siasa wafanye hivyo baada ya Tume ya Nyalali ya Mfumo wa vyama vingi na kutungwa kwa sheria ya vyama vingi vya siasa. Alimeza na kuvumilia kauli ambazo hazikupima staha wala heshima ya mkuu wa nchi.

Hakutaka kupambana na sauti yoyote iliyomkosoa yeye na utawala wake. Katika kitabu chake cha Safari ya Maisha Yangu alichokitwa mwaka 2020, anaeleza jinsi ambavyo alikaa kimya bila kumjibu Mwalimu Nyerere kila alipokuwa akiushambulia utawala wake. Alichagua fungu jema, kutokulumbana na yeyote.



Katika hali ya kawaida, sioni Rais wa Tanzania anayeweza kujizuia kujibu mashambalizi dhidi ya serikali yake na hasa yanapomlenga yeye binafsi. Baada ya Mzee Mwinyi walikuja marais wengine wanne, pamoja na huyo aliyeko sasa.

Tulisikia kauli za ‘mimi sipangiwi’, ‘mimi ni jiwe’, ‘wavivu wa kufikiri’, ‘malofa wakubwa’ nk. Lakini pia Tumeshuhudia watu wakifiliwa biashara zao kwa hila mbaya, tumeshuhudia watu wakipotewa, tumeshuhudia kwa hisia tu, watu wakiteswa kwa sababu waliwaza tofauti na Rais. Mwinyi hakuingia katika mitego hiyo.

Mwinyi ameacha somo, kwamba maisha ni hadithi tu, kila mmoja ajitahidi kuacha simulizi njema kuhusu maisha yake – uvumilivu, huruma na msamaha vilikuwa ngao na kigao katika maisha yake.

Yamkini ndiyo maana Mungu akamkirimu umri ulioshiba miaka, furaha na amani.

Pumzika kwa amani Alhaj Ali Hassan Mwinyi.

Mwandishi wa makala haya ya kukumbuka uongozi wa Rais Ali Hassan Mwinyi, ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Media Brains, Dar es Salaam. Imechapwa hapa kwa ruhusa yake.

DRC/Zambia

Betri kuanza kutengenezwa Congo

Na Mwandishi MAALUM

KIWANDA cha kuchenjua madini kati ya lithium na kutengeneza betri za magari kitajengwa katika ardhi ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) hivi karibuni.

Kuanza kwa ujenzi huo kunafuatia makubaliano ya kimkataba yaliyoingwiwa kati ya nchi mbili; DRC na Zambia, ambapo nchi hizo zitapokea mkopo kutoka taasisi za fedha kwa ajili hiyo.

Inatarajiwa kuwa kazi kubwa inayoanza hivi karibuni ni kuanza upembuzi yakinifu wa kutengeneza betri za magari zinazotumia lithium kwa njia ya kujenga kiwanda katika sehemu ya kusini mashariki mwa DRC.

Mkataba wa utengenezaji wa betri hizo umetiwa saina mbele ya waziri wa Viwanda wa DRC, Julien Paluku Kohongya, na mwenzake wa Zambia, Chipoka Mulenga.

Eneo la takriban hekta za mraba 2000 litajengwa katika Mkoa wa Katanga kwenye mpaka kati ya DRC na Zambia ili kushughulikia sekta hii.

Inakadiriwa kuwa mradi huu unaweza kugharimu dola za Marekani 700,000 na unaweza kufadhiliwa na Benki ya African Import-Export (Afreximbank). Matokeo ya mkopo huo yanategemea kupatikana Agosti, mwaka huu.

Serikali ya DRC imeeleza kuwa mradi huo utaedeshwa katika eneo la mpakani mwa nchi hizo kwa kuwa kuna makubaliano ya kutokuwa na kodi yoyote.

“Tungependa kufanya ubunifu ili kuweza kuendana na teknolojia mpya ya kimataifa - Tunafanya utafiti na maendeleo ambayo yanatuonesha kuwa baadhi ya malighafi ambazo tunazo chini ya ulinzi, zina nguvu zaidi zikitumika kama betri,” alisema Waziri Kahongya.

Ushirikiano huu unalenga kuendeleza



Madini ya lithium

mnyororo wa thamani wa kikanda kati ya nchi zinazolenga soko la magari ya umeme na nishati safi, ambayo inaweza kuleta faida ya mabilioni ya dola kwa nchi zote mbili.

Lithium hutumika katika kutengeneza betri za kisasa kwa teknolojia zinazoitika na ni muhimu kama nishati safi ambayo inaelezwa haiathiri mazingira kwa kiasi kikubwa.

Wiki iliyopita mashapo ya lithium pia yalipatikana kaskazini mwa Tanzania na kampuni ya Marekani ya Titan Lithium Inc., ambayo imekuwa “ikipambana” kusaka madini hayo. Tanzania pia inatajwa kuwa na kiasi kikubwa cha Lithium.

DRC inatajwa kuvutia faida kubwa zaidi kutoka kwa soko la kimataifa, linalowakilisha zaidi ya dola bilioni 800 ifikapo mwaka 2025.

Licha ya operesheni kadhaa haramu za uchimbaji madini nchini DRC, serikali hiyo inadaidai kuwa ni nchi yenye ushindani mkubwa zaidi wa kuzalisha betri za umeme.

Sehemu kubwa ya makala haya yamepatikana kutoka TRT na yamechapishwa hapa kwa kuweka chanzo chake.

Utua wa Rais Mwinyi somo pevu kuongoza

Na Derek MURUSURI

TULIKUWA tunahitimisha ziara ya Rais Ali Hassan Mwinyi katika Mkoa wa Shinyanga mwaka 1993.

Mara, tukaambiwa Rais Mwinyi anataka kupiga picha na wapigapicha wake. Lo! Sisi? Mbio tukaenda. Akatusalimia kwa kutushika mkono, akitushukuru kama baba kwa wanaye.

Alifurahia jinsi habari zake na hasa picha, zilivyokuwa zikipigwa na kuchapishwa katika magazeti mbalimbali hapa nchini. Alikuwa mtu wa kushukuru.

Nami nilikuwa mmoja wa wapigapicha kutoka Idara ya Habari - MAELEZO. Bosi wangu, Raphael Hikororo alinipanga kwenye ziara hiyo.

Rais Mwinyi akatuia, “Njooi tupige picha ya kumbusho.”

Hima tukajongea. Akiwa na mkewe, Mama Sitti Mwinyi, waliketi, sisi wapigapicha tukasinama nyuma yao.

Mpigapicha mmoja akatupiga picha, sisi wapigapicha, tukiwa na Rais Mwinyi na mkewe, Sitti.

Baada ya zoezi hilo, akatuaga.

Siyo viongozi wote wanaojua kushukuru. Fikiria, kiongozi wa nchi anakushukuru kwa kutekeleza wajibu wako, wakati wewe ni mpigapicha tu unayetekeleza wajibu wako. Ni wachache sana.

Mwaka huohuo, nilifanya naye kazi Ikulu kwa wiki mbili na ushee hivi, chini ya Balozi Patrick Chokala.

Kipindi hicho, mpigapicha wake, Henry Isike, alikuwa likizo.

Kuna siku ikahitajika picha na nikasogea kwa ajili ya kutekeleza wajibu wangu, na ili niweze kupata picha nzuri, nilimuomba Rais Mwinyi ajipange kwa kusogea kutoka alipokuwa kwenda hatua chache pembeni. Alikubali kwa unyenyekevu mkubwa.

Baada ya muda huo mfupi hapo, Ikulu, nilisogezwa Ofisi ya Tume ya Mipango,



Rais Mwinyi

iliyokuwa chini ya Ofisi ya Rais. Mwinyi ndiye aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Mipango.

Nilihudhuria kikao kimoja cha tume hiyo katika chumba cha Baraza la Mawaziri, Ikulu, nikashuhudia hekima yake kubwa ya kuendesha vikao. Alimsikiliza kila mwenye hoja, tena kwa umakini mkubwa.

Hakika ulihitaji kuwa karibu na Rais Ali Hassan Mwinyi, ili umfahamu.

Alikuwa kiongozi mnyenyekevu sana, mvumilivu, mwana mageuzi, aliyujenga upya uchumi wa Tanzania, baada ya kuharibiwa sana na vita ya Kagera na hata vita vya harakati za ukombozi wa nchi za kusini mwa Afrika.

Naweza kusema kuwa Mzee Ali Hassan Mwinyi alikuwa Deng Xiaoping wa Tanzania, kwa kipindi kile, kuanzia mwaka 1985. Deng ndiye Baba wa Uchumi wa China.

Aliwahi kupigwa kofi msikitini na kijana mmoja “mjinga tu hivi,” kwa vile alikuwa anajichanganya na raia, lakini akamsamehe.

Rais Mwinyi alishambuliwa sana kwa maneno mengi hadi familia yake ikashutumiwa, lakini, akanyamaza kimya.

Akaendelea kuchapa kazi. Akameza

Hatutakusahau

Utua wa Rais Mwinyi somo pevu kuongoza

Inatoka Uk. 17

kibri chake. Akajishusha.

Hakujitutumua, pakachimbika, hapana! Sio yule Baba. Alitoa kombe kwa mahasimu wake, yeye akaweka nguvu zake kwenye kazi ya kufanya mageuzi ya uchumi wa Tanzania.

Akiwa pia Amir Jeshi Mkuu, Rais Mwinyi – vyombo vyote vya ulinzi na usalama vikiwa chini yake, angeweza kushawishi kuchukua hatua dhiti ya mahasimu wake waadhibiwe, lakini hakutumia nafasi yake wala ‘maguvu’ yake kuwashikisha adabu.

Yeye alikaa kimya. Akasamehe. Tena akafanya kazi na mahasimu wake.

Huyu ni rais aliyeondoa fuleni za kununua sembe. Sabuni za kufulia na dawa za meno zilizokuwa adimu, ambazo zilikuwa zikipatikana kwa magendo tu. Zikajaa madukani.

Watu walifulia nguo sabuni za magwanji, wenye bahati ya kuwa na mipapai, wakatumia majani yake kufulia nguo.

Ni kutokana na haiba yake, Mzee Ali Hassan Mwinyi ni chuo. Yapo mengi sana ya kujifunza kutoka kwake.

Alikuwa kiongozi makini na alijitoa sana kwenye mambo ya kijamii. Yaani, alikuwa karibu na raia aliowaongoza.

Mbali na kufanya mazoezi ya kutembea kila siku, huenda ndiyo siri ya kuishi miaka 98 na miezi 9, takriban miaka 99, alijaaliwa na Mola wake kwa kuonesha maisha ya msamaha, alifundisha Kiswahili kwa kujitolea nchini Uingereza.

Abdullah Ali Hassan Mwinyi, mbunge wa zamani wa Afrika Mashariki, ambaye ni mmoja wa vijana wa Mzee Mwinyi, alipata kunieleza tukiwa Chuo Kikuu cha Cardiff University, Uingereza, kuwa wakati Mzee Mwinyi akiwa Uingereza, alijitolea kufundisha Kiswahili kwa bidii sana.

Ndio maana Baraza la Kiswahili la Taifa (Bakita) na vyombo vya habari

vilimtumia vizuri hapa nyumbani. Alijua, tukiwa na lugha yetu, ikakua na kutumika hata kwenye sayansi na maeneo mengine ya elimu, taifa litapata maendeleo makubwa.

Hili ni somo kubwa la unyenyekevu katika uongozi kwa Watanzania na Waafrika wote.

Nadhani siyo kwa viongozi wa kisiasa pekee, nahisi ni katika maisha ya kila mmoja wetu, iwe nyumbani, ofisini, katika jamii na taifa.

Hata Nabii Issa Bin Maryam, ambaye pia anajulikana kwa jina la Bwana Yesu Kristo, alijishusha na kunyenyekea sana. Kuna nyakati alinyamaza pasipo kusema neno lolote. Hakutumia uwezo wake wa Kiungu kuwasaga adui zake.

Nimeamini, Mwenyezi Mungu huwapenda watu wanyenyekevu, wenye huruma na wenye kumcha.

Basi, ngoja kiongozi wetu, mzee wetu, baba yetu, rafiki yetu, apumzike kwa amani.

Kupitia kwa Rais Mwinyi, nimetambua kuwa kumbe utu ni msingi mkuu wa kiongozi bora na namna njema ya kuishi hapa duniani.

Hata alipolazimika kujiuzulu kwenye nafasi ya waziri wa mambo ya ndani kwa mazingira yasiyomhusu moja kwa moja, ilifika mahali yeye na familia yake wakapatwa hifadhi na rafiki wa karibu.

Hakuwa mbadhirifu. Alikuwa mwadilifu. Lakini hakujisikia vibaya. Muda ulipofika, Mwenyezi Mungu akamkumbuka. Alikuwa mvumilivu sana.

Huyu kiongozi wetu aliyeondoka hakika alikuwa binadamu wa pekee.

Alijaaliwa kipaji cha hwenye kubwa. Kwa kweli ameacha funzo kubwa kwenye kada ya uongozi katika Tanzania na Afrika.

Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na Ardhi, amjaaliye Rais Ali Hassan Mwinyi, pumziko la amani, hadi tutakapoonana mara ya pili.

Ronaldo akiona cha moto Saudia

Na Mwandishi WETU

INAELEKEA mcheza soka wa kimataifa wa Ureno - anayecheza Ligi ya Saudia, Cristiano Ronaldo, sasa amelewa sifa na anakaribia kuharibu kwa kuendekeza vitendo “visivyofaa.”

Wiki iliyopita, Ronaldo anayecheza Timu ya Al-Nassr, alitumia ishara mbaya uwanjani zilizowakera mashabiki.

Ni kutokana na kitendo hicho, Shirikisho la Soka la Saudi Arabia (SFF) nalo limekasirishwa na kitendo cha Ronaldo “kuwatusi” mashabiki wa Klabu ya Al Shabaab na kuchukua hatua za kisheria.

Mashabiki wa Al Shaabab waliokuwa wakipiga kelele za “Messi, Messi, Messi,” kila anapokosa nafasi ya kufunga, ikiwa ni kauli za kumkera, hivyo kukasirika walipoimba jina la Messi

Tayari Kamati ya Nidhamu ya Ligi Kuu ya Saudia – Roshni, imechukua uamuzi wa kumfungia kucheza mechi mbili, huku akipigwa faini kwa kitendo chake.

Katika mchezo huo, timu ya Ronaldo, Al Nassr, ilishinda kwa taabu Al Shaabab kwa mabao 3-2.

Inaelezwa kuwa Ronaldo alikerwa na kelele za timu pinzani na kuamua kufanya alivyofanya – akiwaonesha ishara kwamba “ni watu wasiofaa.”

Baadhi ya vyombo vya habari nchini Saudi Arabia, vinaripoti kuwa gwiji huyo wa zamani wa Manchester United na Real Madrid, asipoadhibiwa huenda atakuwa nyota mwenye “kuenea chuki uwanjani.”

Cristiano Ronaldo ambaye alifunga mojawapo ya mabao ya timu yake, licha ya kuwa mfungaji bora katika ligi hiyo ya Saudia. Hadi sasa ana mabao 22.



Christiano Ronaldo

Kutokana na adhabu dhidi yake, Ronaldo alikosa mechi ya ligi kati ya klabu yake ya Al Nassr na Al-Hazm Alhamisi iliyopita.

Katika ligi timu ya Ronaldo haijaweza kuongoza kwani inapitwa kwa pointi nne dhidi ya Timu ya Al-Hilal ambayo haijapoteza mechi hata moja kwenye ligi hiyo.

Angurumapo Simba...



Timu ya Simba ya Tanzania, imefanikiwa kutinga robo fainali ya Michuano ya Klabu Bingwa Afrika, baada ya juzi - Jumamosi, kuitungua timu kutoka Botswana, Jwaneng Galaxy kwa jumla ya mabao 6-0. Mchezo huo ulichezwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. (Picha na CAF).

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa msunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

